N09/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

88092391

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 3 November 2009 (morning)
Mardi 3 novembre 2009 (matin)
Martes 3 de noviembre de 2009 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.



© International Baccalaureate Organization 2009

**KIFUNGU A**

## UMUHIMU WA KUENDELEZA LUGHA YA KISWAHILI

*Mazungumzo kuhusu umuhimu wa kuendeleza lugha ya Kiswahili katika Afrika ya Mashariki. Mazungumzo yanafanyika na wenyeji watatu kutoka nchi za Afrika ya Mashariki. Wahusika ni: Mukasa (Uganda), Kamau (Kenya) na Mwinyi (Tanzania).*

**Mukasa**: Ndugu zangu ningalipenda tujadili kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili na vipi kimepuuzwa kwa miaka mingi sasa. Je, tufanye nini kulitatua tatizo hili? Nafikiri hapa Tanzania mmepiga hatua kubwa ya kuendeleza Kiswahili.

**Kamau**: Hebu tueleze kidogo kuhusu utumiaji wa Kiswahili hapa Tanzania.

**Mwinyi**: Kuna lugha zaidi ya mia moja hapa Tanzania na nafikiri wazo la nchi ya Tanzania la kuihifadhi na kuiendeleza lugha ya Kiswahili kwa kufanya miradi ya kutengeneza kamusi, kuzipanua kazi za fasihi ni juhudi inayostahili sifa. Kwa vile Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na watu wote nchini Tanzania ni muhimu kiendelee kutumiwa kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi kama ilivyo sasa na hata katika shule za sekondari.


**Kamau**: Kwetu Kenya, wanafunzi wanaanza kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza kwenye shule ya msingi. Kwa hivyo hawapati taabu sana wanapoanza kusoma shule za sekondari upande wa kuzungumza na kuandika Kiingereza lakini upande wa Kiswahili wana matatizo chungu nzima. Wengi wao hawawezi kuzungumza wala kusoma kwa Kiswahili. Isitoshe, hawakipendi Kiswahili sana.

**Mukasa**: Wanafunzi wa Uganda pia wana matatizo ya kuzungumza, kuandika na kusoma Kiswahili. Ni hivi karibuni tu ambapo wameanza kufundisha Kiswahili kwenye shule za msingi. Wao kwa miaka mingi wamekuwa wakitumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia kwenye shule za msingi na sekondari. Wanafunzi wanafanya vizuri sana katika kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu wanaanza kufundishwa kwa lugha hii katika shule za msingi. Hapa Tanzania wanaanza kufundishwa kwa Kiingereza pekee katika shule za sekondari. Lazima ni tatizo au sivyo? Nafikiri wanafunzi hawa wako tayari kuendelea kufundishwa kwa Kiswahili lakini wanarudishwa nyuma kwa kufundishwa kwa lugha nyingine wasiyoizungumza wala wasiyoweza kuisoma na kuiandika kwa urahisi.

**Mwinyi**: Ni kweli kabisa hawafanyi vizuri katika mitihani kwa sababu inawabidi wasome na waandike kwa Kiingereza. Ijapokuwa lugha ya kufundishia katika shule za sekondari ni Kiingereza walimu mara nyingi hueleza mada katika masomo mengi kwa Kiswahili ili wanafunzi waelewe. Na mara nyingine walimu wenyewe hawawezi kujieleza vizuri kwa Kiingereza. Matokeo ni wanafunzi wengi hawafaulu katika mitihani kwa sababu ya kikwazo cha lugha. Mara nyingi hawaelewi maswali.

**Kamau**: Unafikiri tatizo hili litatatuliwa vipi?

**Mwinyi**: Inategemea viongozi wa serikali. Ni muhimu kuwaeleza viongozi hali halisi ya tatizo hili na jinsi ambavyo wanaweza kukikuza Kiswahili zaidi na kukitumia katika shughuli za kielimu katika Afrika ya Mashariki. Wanaweza kukitumia Kiswahili na Kiingereza kwenye shule za kufundishia kwenye shule ya msingi na sekondari.




*Mzalendo*, Mei 2007

**KIFUNGU B**

# NYAMGONDHO WUOD OMBARE

Paukwa!

Pakawa!

Hapo kale paliondokea mvuvi fukara aliyeitwa Nyamgondho Wuod Ombare. Nyamgondho alikuwa mwenyeji wa taarifa ya Gwasi. Hakuwa na mke wala mtoto. Hakurithishwa chochote na babake, kwa hivyo tegemeo lake, kila uchao, lilikuwa uvuvi. Umaskini wa Nyamgondho ulikithiri. Wakati mwingine hakufanikiwa kumvua hata samaki mmoja! Nyamgondho naye hakuchoka kumlilia Muumba wake, "Maulana, Muumba wa mbingu na ardhi, simtupe mja wako. Naomba ulijaze kapu langu."

Siku moja alfajiri, Nyamgondho alikwenda ufuoni, kuangalia nyavu zake, kama kawaida. Lo! Aliona kiroja tosha. Badala ya kawaida ya kuwakuta samaki wakigaragara nyavuni, Nyamgondho alimwona mama mzee amenaswa mumo humo!

Akajiwazia, "Nuksi gani hii? Ni jini au zimwi? Heri nitoroke mara moja…"

"Ee! Bwana, usiniache," ikamtoka sauti yule mwanamke.

"Wewe ni nani?"

"Mimi ni baraka yako. Tafadhali twende kwako ili uweze kuishuhudia baraka yenyewe."

Nyamgondho alikubali shingo upande. Walipofika nyumbani, mama huyo alijengewa nyumba nzuri. Kufumba na kufumbua wakawa mtu na mkewe. Ngoja mali ianze kuingia kwa fujo! Ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na bata. Nyamgondho akawa mume mstahifu. Akakubaliwa katika kikao cha wazee watajika katika taarafa ya Gwasi. Huyu mke wa kwanza alimkubalia kuoa wake wengine. Nyamgondho ati akawa mtu!

Siku hizo, wazee walikuwa na mazoea ya kunywa pombe ya kikoo na kurudi nyumbani usiku wa manane. Siku moja kama hii, Nyamgondho alirudi nyumbani na alipobisha afunguliwe hakujibiwa. Baada ya kuchoshwa na kuchushwa na "ujeuri" huu wa wakeze, alianza kumrushia matusi yule mke wa kwanza. Kwa bahati mbaya, ajuza huyu aligutuka usingizini na kumsikia Nyamgondho akilaani.

"Hata hiki kizee nilichokiokota ziwani kinathubutu kunikaidi? Fungua mlango mara moja au niingie na mlango!"

Mama huyu alikerwa na matusi haya na kumaka, “Nyamgondho, unathubutu kunitusi? Hebu fikiria, ulikuwa nani kabla hujanioa?”

“Nyamaza wewe mtumwa! Huna habari kama nilikuvua ziwani?”

“Ebo! Shika adabu bwana. Mimi ni mamako. Ndimi mboni ya jicho lako.”

“Tazama, sasa naivunjilia mbali ndoa yetu. Naenda zangu. Utajuta.”

Nyamgondho aliyapuuza maneno haya. Alizidi kumdhihaki mkewe na kumhimiza amwondokee pale mara moja. Keshoye, ajuza huyo alifunga safari ya kurudi kwenye ziwa alikovuliwa. Ajabu ni kwamba mali yake yote ilimfuata unyounyo hadi ziwani. Nyamgondho alipotanabahi, alijikuta hana chake. Wakeze walimtoroka alipoishiwa. Hakuruhusiwa tena kushiriki katika kikao cha wazee. Alijaribu kumkimbilia yule ajuza ufuoni lakini hakufua dafu. Nyamgondho alishika tama kwa huzuni, akafa.

W Wallah, *Gateway KCPE Kiswahili* (1996)

**KIFUNGU C**

# KANGA KAMA CHOMBO CHA MAWASILIANO

Kanga au leso ni chombo cha mawasiliano. Mtu hanunui kanga kwa sababu ya rangi zake au nakshi zake tu lakini pia kwa sababu ya ujumbe ambao umeandikwa. Ujumbe huu unaweza kuwa wa kimapenzi, nasaha, elimu au shukrani. Na kuna ujumbe ambao unaonyesha wazi kwamba aliyevaa kanga haelewani na mtu mwingine.

Kanga ni jina la aina ya ndege mwenye rangi nyeusi na madoadoa meupe. Kanga za kwanza zilikuwa na rangi na nakshi kama ya ndege huyo. Wazo la awali la kutengeneza nguo hii lilianza kwa kuunga pamoja kanga sita. Kanga zilikuwa hazina maandishi lakini baadaye misemo ya Kiswahili




ilianza kuandikwa. Kwa kawaida kanga hutumiwa na wanawake ndani ya nyumba na nje ya nyumba. Doti ya kanga huwa kanga mbili za namna moja. Kanga moja ni ya kujifunga kiunoni na kanga ya pili hutandwa kichwani. Wanaume wanaweza kutumia kanga nyumbani tu. Kwa kawaida mwanamke anatumia upande mmoja na mume wake upande mwingine wakati wa kulala.



Pamoja na kujifunga, kujitanda, kuvaliwa na kulaliwa kanga zina matumizi mengi. Kanga zinaweza kutumiwa kama mapazia au kutandika kitanda au kufunika meza. Mtu anaweza kuweka kanga chini na kukalia kama mkeka. Mama mwenye mtoto mchanga anaweza kutumia kanga kumbebea mtoto. Kanga ni zawadi nzuri kwa mume kumpa mkewe, na kwa mtoto kumpa mamake. Wavulana wanaweza kuwapa dada zao zawadi ya kanga na masahib wanawake wanaweza kupeana kanga kama zawadi.


Wakati wa kununua kanga ni lazima mtu aangalie kwa makini maandishi ya kanga. Kwa mfano: kanga zenye maandishi yafuatayo hawezi kupewa mtu yeyote tu: “si mizizi si hirizi kanipenda kwa mapenzi”; “nani kama mama”; “dua njema kwako mpenzi.” Kanga yenye maandishi ya kwanza ni ya ugomvi. Kwa kawaida haitolewi zawadi. Mwanamke akivaa kanga hii, huwa ana ujumbe wa kumpa mtu mmoja mahususi. Kanga yenye maandishi ya pili hupewa mama kama zawadi kutoka kwa watoto kuonyesha mapenzi yao. Na kanga ya tatu kwa kawaida mume humpa mke wake, hupewa pia mama, dada, rafiki anayependwa sana na inaweza kutoka kwa msichana au mvulana.



*Si mizizi si hirizi kanipenda kwa mapenzi*



*Nani kama mama*



*Dua njema kwako mpenzi*

Matumizi ya kanga yanafuata desturi mbalimbali za wenyeji wa Afrika ya Mashariki. Kanga hutumiwa katika sehemu kuu za maisha: arusi, uzazi, na kifo. Bi arusi hupewa doti nyingi za kanga atumie kwa nyumba yake mpya. Na kama akihudhuria sherehe mbalimbali anaweza kujitanda kanga apendayo. Bi arusi hufundishwa na somo yake vipi kutumia kanga hizi.



Magharibi inapoingia, lazima azifukize kwa udi, azipake mafuta ya haliudi, au marashi. Siku za arusi biarusi hufunikwa kanga anapopelekwa chooni na somo yake. Anapojifungua, hasa kama ni nyumbani mkunga humfunika mtoto kwa kanga. Mwanamke akifariki, mwoshaji maiti humwosha na kumkausha kwa kutumia kanga. Kanga hizi baadaye huwa mali ya mwoshaji.



Wanawake wa vijijini hujifunga kanga kiunoni wanapokwenda shambani. Hutengeneza kata ya kuwekea ndoo kichwani wanapokwenda kuchota maji. Wanawake wa dini ya Kiislamu hujifunga na kujitanda kanga wakisali. Wengine hujifunga na kujitanda kutoka nje badala ya buibui, na wengine hujitanda juu ya buibui.

A S Omar, *et al*., *Tuwasiliane kwa Kiswahili* (2007)

**KIFUNGU D**



# MAENDELEO KATIKA MAWASILIANO KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI

Zamani mawasiliano yalihusu kupashana habari kwa njia ya mdomo, na kusafiri nchi kavu kwa kutumia wanyama. Baada ya kugunduliwa maandishi milenia kadhaa zilizopita huko Misri, mambo yalibadilika, si haba. Sasa watu wakawa wanawasiliana kwa njia ya barua, badala ya mdomo kwa mdomo. Upande wa usafiri, vifaa vya mawasiliano pia vilibadilika. Badala ya kuabiri wanyama, watu walianza kusafiri kwa magari. Upande wa baharini, jinsi maendeleo yalivyozidi kupatikana, meli imara zilitengenezwa. Katika uwanja wa kupashana habari, hatua kubwa zilifanyika karne ya 19, 20 na 21, wakati simu, redio, runinga, kompyuta na tarakilishi zilipovumbuliwa.

Ugunduzi wa runinga, komputa na tarakilishi umeifanya dunia kuwa ndogo sana. Leo hii, jambo linapotokea mahali popote ulimwenguni, habari zinafika Afrika siku na saa hiyo hiyo. Kupitia kwa runinga habari zinaenezwa ulimwenguni kote kwa muda mfupi. Kupitia kwa runinga watu wanaonyeshwa, katika nyumba zao, mambo yanavyotendeka mahali popote duniani, jinsi yanavyotendeka, na watu wanayoyatenda. Zaidi, runinga imekuwa chombo mwafaka cha elimu na burudani. Ingawa faida hizi zimeisaidia jamii kwa kiasi fulani kwa upande mwingine zimeleta hasara pia. Runinga imewafanya watu kuwa wazembe. Baadhi ya watu wazima na watoto hukaa muda mrefu wakitazama runinga. Hali hii imeleta matatizo ya kiafya. Runinga pia imechangia katika kuzorota kwa maadili katika jamii za kiafrika hasa upande wa vijana. Kuna baadhi ya filamu zinaonyeshwa katika runinga ambazo zinatukuza vitendo vya kufanya mapenzi kabla ya ndoa, uhalifu, utovu wa nidhamu, matumizi ya dawa za kulevya, kunywa pombe, wizi, ulaghai na maovu mengi. Tabia hizi zimeigwa mno na vijana na zimechangia pakubwa kwenye uzorotaji wa nidhamu na ongezeko la visa vya uhalifu.

Tarakilishi nayo ni mambo mengine tena! Chombo hiki kimefanya mawasiliano kuwa sahali. Kupitia kwa tarakilishi, mtu anaweza kumpelekea ujumbe mwenziwe ambaye yupo mahali popote ulimwenguni. Wataalam wanabashiri kwamba katika karne hii ya 21, haja ya kuandika barua kwa mkono itafifia. Barua zinazopelekwa kwa tarakilishi ndizo zitakazokuwa barua rasmi. Siku hizi watu sio lazima wasafiri maili nyingi ili kufanya mikutano ya kuzungumzia maslahi yao. Kupitia maunganishi ya tarakilishi, watu wanaweza kufanya "mikutano" bila kukutanika wala kuonana.

Kupitia kwa tarakilishi, watu wameweza kufanya biashara bila kuenda dukani. Biashara-meme imekuwa ya kawaida kwa sababu watu wengi siku hizi wananunua na kuuza bidhaa kwa tovuti. Aidha, kupitia kwa tarakilishi, watu wanaweza kusoma hadi kupata shahada bila kuingia mlango wa chuo kinachotoa shahada. Tarakilishi ina baadhi ya mambo yanayovunja moyo. Kuna baadhi ya watu ambao huwahujumu wengine kwa kuharibu progiramu zao. Tarakilishi pia imechangia katika uzorotaji wa nidhamu. Kuna baadhi ya programu kwenye tarakilishi zinazotukuza mapenzi nje ya ndoa, kuavya mimba na dawa za kulevya. Vijana wengi wameacha masomo katika Afrika ya Mashariki kwa sababu ya yale wanayoyaona kwenye tarakilishi. Zaidi ya haya, kumekuwa na ongezeko la wezi wanaotumia tarakilishi kuiba pesa. Vijana wengi wamekuwa wafungwa wa kifaa hiki kutwa kucha na watu wasiojumuika na wenzao. Ili vifaa hivi viweze kuchangia pakubwa kwenye maendeleo katika Afrika ya Mashariki hatua kambambe lazima zichukuliwe kuboresha matumizi yake.

K Njogu, *et al*., *Tanzu za Lugha* (2003)